TANGAZO LA SERIKALI NA 777 la tarehe 18/9/2020

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

SURA 290

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE ZA MWAKA 2020

| | | |
|---|---|---|
| Jina | **1**. | Sheria Ndogo hizi itajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya Njombe za Mwaka 2020. |
| Tafsiri | **2**. | Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale imeelezwa vinginevyo: |
| | | "ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;<br>"afisa mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hizi;<br>"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Njombe;<br>"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri ya kufanya shughuli yoyote iliyobainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;<br>"maeneo maalumu" maana yake ni maeneo yaliyopimwa au yaliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kufanyia shughuli mbalimbali;<br>"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;<br>"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;<br>"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi. | |
| Utozaji wa ada na ushuru | **3.-** | (1) | Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya shughuli zinazofanyika katika eneo la Halmashauri na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwan za la Sheria Ndogo hii. |
| | | (2) | Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri. |
| | | (3) | Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza. |
| | | (4) | Malipo ya ada au ushuru utalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi. |
| | | | |
| Wajibu wa kulipa ada na ushuru | **4.** | Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atatakiwa kulipa ada au ushuru kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi. | |
| | | | |
| Kibali cha Kusafirisha bidhaa | **5.** | Mtu anayesafirisha mazao zaidi ya tani moja kutoka Halmashauri kwenda nje ya Halmashauri atatakiwa kuwa na kibali cha kusafirisha mazao kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi. | |
| Kizuizi | **6.** | Halmashauri inaweza kuweka kizuizi katika eneo lolote ndani ya eneo la Halmashauri kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi. | |
| Ushuru kwa wanyabiashara na watoa huduma wadogo | **7.** | Kila mfanyabiashara mwenye kitambulisho cha wafanyabiashara na watoa huduma wadogo kilichotolewa na selikali hatatozwa ushuru wa aina yoyote katika biashara yake ambayo ilikidhi vigezo vinavyotakiwa kuwa na kitambulisho hicho. | |
| Muda wa kukusan | **8.-** | (1) | Muda wa kukusanya ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili |

| | | | |
|---|---|---|---|
| ya ada na ushuru | | | kamili jioni. |
| | | (2) | Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ushuru baada ya saa kumi na mbili jioni. |
| | | (3) | Malipo ya ada na ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru. |
| | | (4) | Malipo ya ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika. |
| Usimamizi wa Sheria Ndogo | **9.-** | (1) | Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri. |
| | | (2) | Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ada au ushuru. |
| | | (3) | Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada. |
| | | (4) | Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi. |
| | | (5) | Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa na Halmashauri au Wakala. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| Uteuzi wa Wakala | **10.-** | (1) | Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi. | |
| | | (2) | Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa: | |
| | | | (a) | kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hizi; |
| | | | (b) | kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri. |
| Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa | **11.** | Bila ya kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi, afisa mwidhiniwa wakati wa muda wa kazi anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa lengo la kukusanya ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi. | | |
| | | | | |
| Makosa na adhabu | **12.-** | (1) | Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo- | |
| | | | (a) | atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii; |
| | | | (b) | atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru; |
| | | | (c) | atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii; au |
| | | | (d) | ametoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru. |
| | | (2) | Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne. | |
| Kufililisha kosa | **13.** | Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria | | |

| | | |
|---|---|---|
| | | Ndogo hii kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi laki tano endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum na kulipa ada au ushuru anaodaiwa kama iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi. |
| | | |
| Kufutwa kwa Tangazo la Serikali Na. 471 la Mwaka 2015 | **14.** | Sheria Ndogo (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe za mwaka 2015 zinafutwa. |

## JEDWALI LA KWANZA

***(Limetungwa chini ya Kifungu 3 (1))***

### I. ADA YA KUKODISHA/KUPANGISHA MALI ZA HALMASHAURI

| Na. | Huduma | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya mikutano/ vikao na sherehe kwa mashirika na Taasisi za Serikali. | 200,000/= |
| 2 | Matumizi ya ukumbi kwa mashirika na watu binafsi | 300,000/= |
| 3 | Kukodi Gari: Magari madogo na Magari makubwa | Kwa mujibu wa bei ya soko |
| 4 | Vifaa (Trekta, Total station, GPS na kadhalika) | Kwa mujibu wa bei ya soko |
| 5 | Vibanda vya biashara mzunguko wa Stendi | Kwa mujibu wa bei ya soko |
| 6 | Vibanda vya biashara sokoni | Kwa mujibu wa bei ya soko |
| 7 | Kokodi shamba la Halmashauri | 50,000/= kwa ekari kwa msimu |
| 8 | Kupangisha nyumba/Majengo ya Halmashauri | Kwa mujibu wa bei ya soko |

### II. ADA NA USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO

| *Na* | *Zao* | *Kiwango Kwa Shilingi* |
|---|---|---|
| 1 | Viazi mviringo | 3% ya bei ya kununulia |
| 2 | Vitunguu maji/Matunda/Karoti/Kabichi/ Nyanya | 3% ya bei ya kununulia |
| 3 | Maharage/ Karanga / Mchele/Ngano | 3% ya bei ya kununulia |
| 4 | Mihogo/Viazi vitamu | 3% ya bei ya kununulia |
| 5 | Mahindi/Alizeti/Uwele/Mtama/Mpunga/ | 3% ya bei ya kununulia |
| 6 | Dengu/Choroko | 3% ya bei ya kununulia |

| | | |
|---|---|---|
| 7 | Mbogamboga | 3% ya bei ya kununulia |
| 8 | Vitunguu Swaumu/Tangawizi | 3% ya bei ya kununulia |
| 9 | Nanasi | 3% ya bei ya kununulia |
| 10 | Tikiti | 3% ya bei ya kununulia |

## III. ADA NA USHURU MAZAO YA BIASHARA

| *Na.* | | *Zao* | *Kiwango/ushuru* |
|---|---|---|---|
| 1 | | Maua | 3% ya bei ya kununulia |
| 2 | | Pareto iliyokaushwa | 3% ya bei ya kununulia |
| 3 | | Kahawa | 3% ya bei ya kununulia |
| 4 | | Chai | 3% ya bei ya kununulia |
| 5 | | Mazao Mengine ambayo hayakutajwa yanayofanana na Na. 1 hadi 4 | 3% Bei ya soko |

## IV. ADA YA HUDUMA ZA UKAGUZI WA NYAMA NA MACHINJIO

| *Na* | *Ada/ushuru* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| **1** | Ada ya Machinjio na Ukaguzi wa nyama kwa kila Ng'ombe atakayechinjwa | 3,000/= kwa siku |
| **2** | Ada ya Machinjio na Ukaguzi wa nyama kwa kila Kondoo na Mbuzi atakayechinjwa | 1000/= kwa siku |
| **3** | Ada ya machinjio na Ukaguzi wa nyama kwa kila nguruwe | 2000/= kwa siku |
| **4** | Kuwamba na kukausha ngozi<br>(a) Ng'ombe | 1000/= ngozi |
| | (b) Mbuzi, Kondoo | 500/= kw a ngozi |
| **5** | Ada ya ushuru wa Wachoma nyama ya Ng'ombe Mbuzi, Kondoo, (Mnadani). | 500/= kwa mfugo |
| **6** | Ada ya uogeshaji mifugo (josho) | 200 kwa mfugo |
| **7** | Kibali cha machinjio | 3000 kwa mfugo |
| **8** | Ada ya kusafirisha ngozi<br>(a) Ng'ombe | 500/= kwa ngozi |
| | (b) Mbuzi, Kondoo | 500/= kwa ngozi |
| **9** | Ada ya chapa ya mifugo kama ng'ombe n.k | 500 kwa mfugo |
| **10** | Ada ya chanjo ya mifugo | Inategemea bei ya chanjo |

## V. USHURU WA MAUZO YA MIFUGO MINADANI

| *Na* | *Aina ya Mnyama* | *Tozo* |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 5000/= kwa ng'ombe |
| 2 | Mbuzi | 1500/= kwa mbuzi |
| 3 | Kondoo | 1500/= kwa kondoo |
| 4 | Ushuru wa Kuku | 1000/= kwa tenga |
| 5 | Punda | 1500/= kwa punda |

## VI. ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI, BURUDANI NA MICHEZO

## A. ADA ZA SHUGHULI BURUDANI NA MICHEZO

| ***Na*** | ***Ada/Ushuru*** | ***Kiwango*** |
|---|---|---|
| 1 | Kibali cha ngoma kubwa | 100,000/= kwa onesho |
| 2 | Kibali cha ngoma ndogo | 20,000/=kwa onesho |
| 3 | Mbio za Baiskeli | 20,000/= kwa mchezo |
| 4 | Kibali cha kuchezesha disco, Maonyesho ya bendi, Sanaa za maonyesho (Sinema, video, maigizo, sarakasi, ngoma n.k | 50,000/= Kwa tukio |
| 5 | Kibali cha Mechi za Mipira | 10,000/=kwa ligi<br>5000/= kwa mechi |
| 6 | kibali ya video au sinema | 60,000/= kwa onesho |
| 7 | Bahati nasibu ndogo ndogo (fete) | 50,000/= kwa mchezo |
| **Na.** | ***B.*** **Ada za Shughuli za Tiba za Asili** | |
| 1 | Waganga toka nje ya Wilaya | 120,000/= kwa Mwaka |
| 2 | Waganga maarufu ndani ya Wilaya | 100,000/= kwa Mwaka |
| 3 | Waganga wadogo ndani ya Wilaya | 50,000/= kwa Mwaka |
| 4<br>5 | Kibali cha kuuza dawa za asili<br>Ada ya mizizi | 50,000/= kwa Mwaka<br>20,000/= kwa Mwaka |

## VII. ADA NA USHURU WA STENDI NA MAEGESHO KWA MAENEO YALIYOTENGWA

| *Na* | *Chombo cha Usafiri* | *Ushuru wa Maegesho* |
|---|---|---|
| 1 | Pikipiki iliyosajiliwa kwa Biashara katika maeneo yaliyotengwa | 1,000/= kwa siku |
| 2 | Tax na pick-up | 1000/= kwa siku |
| 3 | Malori | 5,000/= kwa siku |
| 4 | Kulaza Gari Kituoni | 2000/= kwa siku |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | Ushuru wa kituo cha mabasi/stendi<br>(a) Mabasi makubwa abiria 45 na zaidi<br>(b) Mabasi yanayobeba abiria 24 hadi 44<br>(c) Mabasi madogo ya chini ya abiria 44 | 2,000/= kwa siku<br>1,500/= kwa siku<br>1000/= kwa siku |
| | | |

### VIII. ADA YA MATANGAZO YA BIASHARA/PROMOSHENI

| *Na* | *Aina ya Tangazo* | *Kiwango cha ushuru kwa mwaka* |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | Kibali cha muziki/Disko | 50,000/= kwa siku |
| | | |
| | Matangazo ya vipaza Sauti/ Magari na Promosheni | 50,000/= kwa siku |
| | | |

### IX. ADA YA UPIMAJI WA ARDHI NA VIBALI VYA UJENZI

| Na | *A. Ada ya Kibali cha Ujenzi/ Upimaji* | *Kwa kibali* |
|---|---|---|
| 1 | Mnara wa simu | 500,000/= |
| 2 | Jengo la Ghorofa moja na kuendelea | 200,000/= |
| 3 | Nyumba za Biashara | 50,000/= |
| 4 | Nyumba ya Makazi | 20,000/= |
| 5 | Kituo cha mafuta | 250,000/= |
| 6 | Majengo ya Taasisi Binafsi | 150,000/= |
| 7 | Maghala na Bohari. | 100,000/= |
| 8 | Ujenzi wa Uzio | 100/= kwa "Sq meter |
| 9 | Majengo ya Ibada | 100,000/= |
| 10 | Vituo vya Utalii/Mapumziko | 250,000/= |
| 11 | Majengo ya Viwanja | 1,000,000/= |
| 12 | Viwanda Vidogo Vidogo vya Huduma | 200,000/= |
| 13<br>14 | Ada ya uchunguzi wa ramani za ujenzi<br>Kibali cha ujenzi wa planti | 10,000/=<br>1,000,000/= |
| *Na* | *B. Ada ya mabadiliko ya Matumizi ya Jengo* | *Kwa kibali* |
| 1 | Nyumba ya kuishi na biashara | 40,000/= |
| 2 | Nyumba ya Biashara | 60,000/= |
| 3 | Nyumba ya kuishi | 30,000/= |
| 4 | Ghorofa | 150,000/= |
| 5 | Kiwanda, Bohari, Ghala | 100,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Mabadiliko ya matumizi ya ardhi (Makazi) | 20,000/= |
| 7 | Mabadiliko ya matumizi ya ardhi (Biashara) | 50,000/= |
| | | |
| *Na.* | *C. Ada za huduma ya ardhi* | *Kiwango* |
| 1 | Mchoro wa upimaji | 10,000/= kwa kila mchoro |
| 2 | Kutambua eneo (Plot identification) | 10,000/= kwa kila plot |
| 3 | Kurudishia mawe yanaonesha mipaka (Beacon replacement) | 5,000/= kwa kila jiwe |

### X. USHURU WA HOTEL (Hotel Levy)

| *Na* | *Aina ya Biashara* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1. | Hotel/Nyumba ya kulala wageni | 10% ya mauzo kila chumba kwa siku |

### XI. ADA NA USHURU WA HUDUMA MBALIMBALI

| *Na.* | *Ada* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya kupima afya kwa wahudumu wa Baa, Hoteli na Migahawa na maeneo mengine ya kutoa huduma za vyakula au vinywaji kwa umma. | 5000/= kwa miezi sita (6) |
| 2 | Ushuru wa kuhifadhi wanyama waliokamatwa kwa kuzurura ovyo. | 3000/= kwa mnyama kwa siku |
| 3 | Faini ya Uchafu na kutovaa sare kwa wahudumu wa Bar/ Mgahawa/Hotel na maeneo mengine ya kutoa huduma za vyakula au vinywaji kwa Umma | 20,000/= kwa siku |
| 4 | Ada ya usajili vikundi vya jamii | 10,000/= kwa ombi |
| 5 | Ada ya maombi ya hati ya ukomo wa madeni | 50,000/=kwa ombi |
| 6 | Ada ya kukagua hesabu za shule za Sekondari Binafsi | 100,000/=kwa ombi |
| 7 | Ada ya pango la ardhi kwa wamiliki wa maeneo yaliyopangishwa Minara ya Simu | 5% ya alicholipwa |
| 8 | Kukodisha vifaa vya muziki vya Halmashauri | Kwa mujibu wa bei ya soko |
| | | |
| 9 | Vitabu vya ushuru wa Hotel/nyumba ya kulala wageni | 15,000/= kwa kitabu |
| 10 | Leseni ya Biashara ya Samaki | 30,000 kwa leseni |
| 11 | Mialo ya kuchenjulia dhahabu | 20,000 kwa kila mwalo kwa mwezi |
| 12 | Kibali cha kufanya utafiti wa madini | 1,000,000/= Kwa mwaka |

| | | |
|---|---|---|
| 13 | Ushuru wa malori yanayojihusisha na shughuli za uchimbaji wa madini;-<br>a. Malori yanayofanya shughuli ndani ya mgodi (yasiyotoka/kuingia eneo la mgodi)<br>b. Malori yanayotoka nje ya eneo la mgodi | 30,000 kwa mwezi<br>1,000/= kwa tripu |
| 14 | Ushuru wa Halmashauri kwa kila "*plant" mtambo* wa uchenjuaji. | 3,500,000/= kwa mwaka |
| 15 | Karasha | 20,000/= kwa mwezi |
| 16 | Leseni ya kumiliki gobore | 3,000/= kwa mwaka |
| 17 | Ushuru wa tofali za kuchoma | 20/= kwa kila tofali |
| 18 | Ada ya mikataba | 3% katika kila hati ya malipo ya mkataba |

## XII. ADA YA MAOMBI YA ZABUNI

| | *Ombi* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1 | Zabuni ya ushuru Minada/masoko na mazao | 100,000/= kwa kila ombi |
| 2 | Zabuni ya kutoa huduma na kazi mbalimbali | 100,000/= kwa kila ombi |
| | | |

## XIII. USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Na | Aina ya Madini | Tani | Kiwango Tsh. |
|---|---|---|---|
| 1 | Mchanga/Kokoto /mawe kifusi | 1-3 | 3000/= |
| 2 | Mchanga /Kokoto/mawe/kifusi | 3-5 | 5,000/= |
| 3 | Mchanga /kokoto/mawe/kifusi | 5-10 | 5,000/= |
| 4 | Mchanga /kokoto/mawe/kifusi zaidi ya | 10 | 1000/= kwa kila tani itakayoongezeka |

### XIV. USHURU WA KUFANYA BIASHARA KATIKA MAGULIO/MINADA

| Na | Aina Ya Bidhaa | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Mitumba kwa tandiko | 1,000/= kwa mfanyabiashara |
| 2 | Vyombo vya nyumbani kwa tandiko | 1,000/= kwa mfanyabiasha |
| 3 | Nguo za dukani | 1,000/= kwa mfanyabiahara |
| 4 | Biashara nyinginezo ambazo hazikutajwa | 1,000/= kwa mfanyabiashara |
| 5 | Samaki, urembo,viatu,nguo za madukani | 500/= kwa siku |
| 6 | Vileo | 1000/= kwa siku |

### XV. USHURU WA KUSHUSHA MIZIGO KATIKA ENEO LA SOKO LOLOTE LILILOTENGWA NA HALMASHAURI

| Na | Aina ya chombo cha usafiri | Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Uzito wa kuanzia tani 1-5 | Tsh.3,000/= |
| 2 | Uzito wa kuanzia tani 6-10 | Tsh.7,000/= |
| 3 | Uzito wa kuanzia tani 11-20 | Tsh.15,000/= |
| 4 | Uzito wa kuanzia tani 20-50 | Tsh.20,000/= |

### XVI. ADA YA KUKODISHA MITAMBO NA MAGARI YA HALMASHAURI BILA POSHO YA DEREVA

| Na | Aina gari/mtambo | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Kukodi tipper | Kwa mujibu wa mkataba |
| 2 | Kukodi boza | 300,000/= kwa kila baada ya masaa nane |
| 3 | Greder | 650,000/= kwa kila baada ya masaa nane au chini yake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. |
| 4 | Ukodishaji wa magari mengine | Kwa mujibu wa mkataba. |

### XVII. ADA YA KUKATA MTI NA MASHINE

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya kukata mti | 200/= kwa mti |
| 2 | Mashine ya kukatia mti | 50/= kwa mti |

## XVIII. USHURU WA HUDUMA KWA BIASHARA KUBWA, NDOGO NA ADA YA LESENI YA BIASHARA

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Ushuru wa huduma kwa biashara ndogo | 4500/= kwa mwezi |
| 2 | Ada ya maombi ya leseni (fomu) | 2000/= kwa mwaka |
| 3 | Ada ya Leseni | Italipwa kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Serikali kutegemeana na aina ya biashara |
| 4 | Ushuru wa huduma kwa biashara kubwa | kiwango kisichozidi asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) kutokana na uzalishaji wa bidhaa, kazi na huduma zinazofanyika ndani ya eneo la Halmashauri ukiondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na Kodi ya bidhaa (excise duty). |

## XIX USHURU WA MAZAO YA MISITU

| | | |
|---|---|---|
| **1** | Magogo | 4,000/= kwa kila tani moja |
| **2** | Leseni ya mbao | 100,000/= kwa mwaka |
| **3** | Kukausha mbao | 100/= kwa kila ubao |
| **4** | Mbao laini | 200/= kwa kila ubao |
| **5** | Mbao ngumu | 200/= kwa kila ubao |
| **6** | Nguzo(untreated) | 3,000/= kwa kila nguzo |
| **7** | Milunda | 150/= kwa kila mlunda |
| **8** | Mkaa | 1,000/= kwa Kg 1-30<br>2000/= kwa kg 31 na zaidi |
| **9** | Nguzo(treated) | 5% ya bei ya kununulia |
| | | |

JEDWALI LA PILI

*(limetengenezwa chini ya Kifungu cha 5*)

KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAZAO YANAYOZIDI TANI MOJA

Kibali kinatolewa kwa
Ndugu…………………………………………………………………………….
Mmiliki wa leseni au kitambulisho cha mjasiliamali
Na………………………………. toka ………………………………….
Kwa ajili ya kusafirisha mazao toka Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwenda …………………
Kwa bidhaa yenye maelezo yafuatayo:

| Aina ya mazao yanayosafirishwa | Ujazo wa mazao | Ada na Ushuru uliolipwa Halmashauri | Na. ya risiti | Mahali mazao yanapotoka | Mahali mazao yanapopelekwa | Tarehe ya kusafirisha mazao |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |

Kibali cha kusafirisha mazao kimetolewa leo hii tarehe………. mwezi………. mwaka………...

Jina la Afisa mwidhiniwa……………………
Saini………………….
Cheo……………………
Jina la mwombaji wa kibali……………………………………………………………
Saini…………………….
Tarehe…………………….

JEDWALI LA TATU

*(limetengenezwa chini ya kifungu cha 13)*

HATI YA KUFILILISHA KOSA

Mimi ………………………………………………………………… nakiri KWA HIYARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Njombe, kwamba tarehe …… ya mwezi ………………. mwaka ………………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …………………………… cha Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe za Mwaka 2020.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, niko tayari kulipa faini ya kiasi cha ……………………………………………………………………….. pamoja na ada au ushuru ninaodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAYO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya mwezi……… mwaka ……………………….

Jina…………………………………… Saini………………………………

Mbele ya:

Jina: ……………………………………………

Cheo: …………………………………………….

Saini: …………………………………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililotolewa katika kikao cha baraza la madiwani cha tarehe 31 /7/2019 na kushuhudiwa na:

……..………………………
ALLY J. ALLY
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.*

……………………………..
VALENTINO A. HONGOLI
*Mwenyekiti wa Halmshauri*
*Halmashauri ya Wilaya ya Njombe*.

**NAKUBALI**

Dodoma,
1st September, 2020

………………………………
SELEMANI S. JAFO (MB)
Waziri wa Nchi-0R-TAMISMI